



TAARIFA KWA UMMA

MATUMIZI YA KITUFE CHA UTAMBUZI WA DEREVA (i-BUTTON) KWA MABASI YA 'SPECIAL HIRE'

Dar es Salaam, Tarehe 31 Desemba, 2024

Kwa mujibu wa kanuni ya 20(b) ya Kanuni za Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini za Magari ya Kukodi za mwaka 2020, Mabasi Maalumu ya Kukodi (Special Hire) yanapaswa kuunganishwa na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS). Mfumo huo huwezesha Mamlaka kumtambua dereva anayeendesha gari husika endapo dereva huyo atasajiliwa na kutumia Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i-button).

Aidha, Kanuni ya 9(2) ya Kanuni za Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini za Uthibitishaji Madereva na Usajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Kibiashara Mamlaka ina jukumu la kuainisha magari yanayopaswa kutumia Kitufe cha Utambuzi wa Dereva ambapo Mabasi Maalumu ya Kukodi ni miongoni mwa magari yaliyo ainishwa. Pia Kanuni ya 9 (3) inamtaka dereva aliyepewa Kitufe cha Utambuzi kuhakikisha kitufe hicho kiko salama na kutompatia mtu mwingine yeyote.

Hivyo, Mamlaka inawakumbusha madereva na wamiliki wa Mabasi Maalumu ya Kukodi kuzingatia matumizi sahihi ya Kitufe cha Utambuzi wa Dereva. Madereva wasio na kitufe hicho wafike ofisi za LATRA zilizo karibu ili kusajiliwa na kuunganishwa kabla ya tarehe 12 Januari, 2025. Ili kurahisisha kazi hiyo, Mamlaka itafanya usajili wa Vitufe vya Utambuzi wa Dereva kwenye baadhi ya maeneo ya barabara ambayo mabasi husimama.

Salum Pazy
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano